

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE

06 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE – TAREHE 06 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**200. MHESHIMIWA MWANTUM DAU HAJI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa Watu Wenye Ulemavu.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**201. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL
MNZAVA (KOROGWE VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya upungufu wa Watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe hasa kwenye Idara za Afya, Elimu na Kilimo.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**202. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA
GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Viwanda vya *General Tyres* na *Pharmaceutical Industries Ltd.* ili kuongeza ajira na upatikanaji wa dawa nchini.

WIZARA YA MAJI:

**203. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS
MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia maji Wananchi walio katika Vijiji ambavyo havifikiwi na Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria katika Jimbo la Tabora Kaskazini.

**204. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL
KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kujenga miundombinu ya maji katika Vijiji vya Kipunda, Minyughe, Ighombwe, Makungu, Mpetu, Magungumka na Mnang'ana.

V. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.



**DODOMA
06 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**